
# SUA MATUKIO YA MWEZI





## AGOSTI, 2019
## "ARDHI NI HAZINA"

## ZIARA YA MAKAMU WA RAIS SUA.....





## RAIS WA AFRIKA KUSINI AISHUKURU TANZANIA...





# RAIS WA AFRIKA KUSINI AISHUKURU TANZANIA.



Rais wa Afrika ya Kusini Cyril Ramaphosa ameishukuru Serikali ya Tanzania kwa kushiriki katika harakati za ukombozi wa Afrika Kusini kwa vitendo na kuahidi kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo katika kuboresha miundombinu ,kubadilishana uzoefu na kukuza Teknolojia . Rais huyo amesema hayo wakati alipotembelea SUA na kuongeza kuwa anapoitazama Mazimbu anaiona wazi Afrika kusini ndani ya Tanzania na kwamba Tanzania ni nchi ya kipekee ilivyoweza kuhamasisha umoja na mshikamano kwa nchi za afrika wakati wa ukoloni na utawala wa kibaguzi.



Aidha ameongeza kuwa, Tanzania imegharimika kiuchumi kwa kuwa ililazimika kuharibu miundombinu yake hasa katika maeneo ya kusini ili kuzuia watawala wa kibaguzi kuingia Tanzania na kuwavamia wapigania uhuru na ukombozi waliokuwepo wakimemo wa ANC kutoa afrika kusini.



Kwa upande wake Waziri Mkuu wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa amesema eneo la Mazimbu lina uhusiano mkubwa na historia ya nchi hizo mbili kwani eneo hilo limebeba historia muhimu ya kumbukumbu ya vuguvugu la ukombozi wa nchi Ya Afrika ya Kusini Nae Makamu wa Mkuu wa Chuo cha Sokoine cha Kilimo SUA Prof . Rafael Chibunda amemuelezea Rais Ramaphosa na ujumbe wake kutoka afrika kusini historia ya chuo na namna ambavyo Baba wa Taifa Mwalimu Julias Kambarage Nyerere aliona umuhimu wa kutoa majengo hayo ya wapigania uhuru kwa chuo hicho kwa ajili ya maendeleo ya kilimo nchini . Rais Ramaphosa ametembelea katika maeneo mbalimbali ndani ya Kampasi ya Solomoni Mahlangu walipokuwa wakiishi wapigania uhuru, eneo la makabuli ambapo rais huyo ameweka shada la maua na kupanda mti ikiwa ni ishara ya muendelezo wa kumbukumbu ya uhusiano kwa vizazi vijavyo.



# MAMA SAMIA AITAKA SUA KUSIMAMIA MISINGI YA MWL.NYERERE

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amekitaka chuo kikuu cha sokoine cha kilimo SUA kuendelea kusimamia misingi ya kuanzishwa kwake iliyowekwa na Hayati Baba wa Taifa Mwl Julius Kambarage Nyerere.



Mhe. Makamu wa Rais ameyasema hayo wakati akizungumza na wanajumuiya wa SUA, wakazi wa Mkoa wa Morogoro na Viongozi wa Mashirika na taasisi binafsi na za serikali kwenye hafla fupi ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa maabara mtambuka katika chuo kikuu cha kilimo SUA.



“ Katika hotuba ya Marehemu baba wa Taifa wakati wa uzinduzi wa Chuo hicho alisema bayana malengo ya uanzishwaji wa chuo cha SUA hivyo malengo yake ni lazima Serikali na Wana SUA kuendelea kuyaishi ili yaweze kusaidia kujibu changamoto mbalimbali za wakulima na kuondoa Adui Umasikini” Alisema Mhe. Samia.

Makamu huyo wa Rais wa Jmahuri ya Muungano wa Tanzania amesema Pamoja na kufundisha na kufanya tafiti nzuri zenye kusaidia kuongeza tija kwa wakulima lakini ameshauri SUA kuongeza somo la uzalendo kwenye masomo yake ili wahitimu wanaotoka hapo wakafanye kazi kwa weledi na uzalendo kusaidia kuboresha maisha ya wakulima, Wafugaji na wavuvi nchini.

Awali Mwenyekiti wa baraza la Chuo Jaji Mkuu Mstaafu wa Tanzania Mhe. Othman Chande apongeza ushirikiano mkubwa ambao baraza lake linaupata kwa Viongozi wa SUA na hivyo kusaidia kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo chuoni hapo ingawa chuo kinakabiliwa na uhaba wa fedha za maendeleo.

“ Kutokana na umuhimu wa Chuo hiki kwa Taifa naomba Serikali iongeze bajeti kwa vyuo vyote vya Umma hasa SUA ambayo inategemewa na zaidi ya asilimia 75 ya watanzania” Alisisitiza Mhe. Chande.

Hata hivyo amemuomba Makamu wa Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan kufikisha salama za shukrani kwa Rais Dkt. Magufuli kwa jitihada zake za kuendelea kukisaidia chuo hiki muhimu kwa nchi na kumuomba Makamu wa rais kukisaidia chuo hicho muhimu kwa Taifa.

Kwa upande wake Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Mhe. Jaji Mstaafu Joseph Sinde Warioba amesema chuo cha SUA ndicho kinachotegemewa sana kuboresha maisha ya watanzania wengi hasa kwakuwa ndio uti wa mgongo wa Matanzania.

Jaji Mstaafu Warioba amesema maadui wata-

tu ambao Baba wa Taifa alipambana nao Ujinga na Maradhi tumefanikiwa kama nchi kuwakimbiza lakini adui Umasikini ndio bada anaisumbua Tanzania na wananchi hasa wale wa vijijini. ‘‘ Chuo kikuu cha Sokoine kina mchango mkubwa katika kusaidia kuondokana na adui huyu ambaye bado anaendelea kuwatesa wanzania endapo Matunda ya kazi za tafiti zinazofanywa chuoni hapa zitatumiwa vizuri na serikali” Alisema Mkuu wa Chuo Jaji Mstaafu Warioba.

Akitoa taarifa ya chuo na ujenzi wa jengo hilo Makamu wa Mkuu wa Chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Prof. Raphael Chibunda ameipongeza serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa jitihada kubwa inazozifanya katika kuboresha miundimbinu ya chuo kwa kutoa fedha maendeleo vizuri toka ilipoingia madarakani na hivyo kwezesha kutekeleza miradi mbalimbali ya chuo ikiwemo maabara hiyo.

Prof. Chibunda amesema Jengo hilo la ghorofa tatu litakuwa na maabara nane na vyumba vya madarasa nane ambavyo kwa ujumla linaweza kuchukua wanafunzi 2400 kwa wakati mmoja.

‘‘Namshukur Rais John Pombe Magufuli kwa kutekeleza ahadi yake ya kutoa matrekta kumi katika ziara yake aliyoifanya Mwaka jana chuoni kwetu pamoja na kutoa fedha za ndani za serikali kujenga jengo hili la maabara mtambuka” Alisema Prof. Chibunda.

Akizungumza kabla ya kumkaribisha mgeni rasmi WAZIRI wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Joyce Ndalichako ameiahukuru serikali ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuboresha elimu ya Tanzania kwa kuzisaidia juzi Presha shule zote maalufu nchini ili ziweze kutoa elimu bora kwa watanzania.

## SERIKALI KUTUMIA TAFITI ZA WANAFUNZI KUINUA SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeandaa Mpango Maalumu wa kukusanya Tafiti za wanafunzi wa Shahada ya Uzamili, Uzamivu na Kwenye Taasisi zingine na mafunzo na utafiti ili wizara ifanyie kazi mapendekezo ya tafiti hizo na kusaidia kuboresha sekta ya Mifugo na Uvuvi nchini.

Mpango huo umebainishwa na WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhanga Mpina wakati akizungumza na watafiti na wanahabari kwenye banda la Maonesho ya Wakulima nanenane kanda ya Mashariki yanayofanyika kwenye Viwanja vya Mwl Julius Kambarage Nyerere Mjini Morogoro.

‘‘Kuna tafiti nyingi na nzuri zenye mapendekezo muhimu sana katika kuboresha sekta ya Mifugo na Uvuvi nchini zinazofanywa katika chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA na kwenye taasisi zingine za mafunzo na utafiti lakini zinaishia makabatini na haziwafikii walengwa na kutoa tija kwa taifa” Alisema Mhe. Mpina.



WAZIRI huyo wa Mifugo na Uvuvi amesema wanasayansi na wanafunzi hao wanafanya kazi nzuri na kubwa lakini zinawasaidia wao tuu kupata shahada na kupanda madaraja makazini lakini mapendekezo ya tafiti zao hayatumiki na hivyo kusema kuwa wakati umefika kazi hizo nzuri zilisaidie taifa, wafugaji na wavuvi.

Mhe.Mpina amesema tayari ameshatoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa utafiti na mafunzo katika Wizara yake kuratibu Mpango huo ambao anaamini utasaidia sana kuboresha sekta na kuiuza uchumi wa taifa na nchi.

Mhe. Mpina aliongeza kuwa “ Tutazikusanya na kuzichambua zote kila Mwaka na kuyafanyia kazi mapendekezo mazuri yanayotolewa na watafiti hao na wanafunzi na pale itakapolazimika kubadirisha kanini, sheria basi tutafanya hivyo kabdri mapendekezo hayo yatakavyosema ili zilisaidie taifa letu, Kazi za wanafunzi hao zisipotee bure bali waone zikisaidia jamii na taifa kusonga mbele kwa kuleta tija”.
Kwa upande wake Kaimu Makamu wa Mkuu wa Chuo Dkt. Samweli Kabote amesema ni kweli tafiti zinazofanywa ni nyingi kila Mwaka na zitaleta tija sana endapo hilo gap likiondoka kati ya wizara na vyuo.

Dkt. Kabote amemuahidi Waziri Mpina kuwa Chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA kipo tayari kushiriki kwenye Mpango huo wa Wizara ili tafiti hizo zilete tija inayokusudiwa kwa Taifa na wafugaji.
Chuo Kikuu cha Sokoneycha Kilimo SUA kinashiriki kwenye maonesho ya Wakulima nanenane Kitaifa Mkoani Simiyu pamoja na Kikanda Mkoani Morogoro.

## RAIS KIKWETE APONGEZA JITIHADA ZA SUA KUBORESHA KILIMO

Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete amepongeza kazi kubwa inayofanywa na Watafiti na hivyo kuja na mbinu na teknolojia mpya kila Mwaka ambazo zinajibu changamoto mbalimbali za wakulima na hivyo kuongeza tija.

Hayo ameyasema wakati alipotembelea Banda la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA kwenye maonesho ya Wakulima nanenane Kanda ya Mashariki yanayofanyika kwenye Viwanja vya Mwl. Julius Kambarage Nyerere Mkoani Morogoro.



Mhe. Dkt. Kikwete amesema kila Mwaka kwenye maonesho ya Wakulima nanenane anaona mbinu na teknolojia mpya hivyo hii inaonesha kuwa kuna maendeleo kwenye tafiti na Mashamba ya wakulima.
“ Changamoto za wakulima ni nyingi sana tunaweza ziongea siku nzima lakini kubwa hizi za wadudu na mabadiliko ya tabia nchi ni lazima watafiti Wetu wawndelee kuzishughulikia maana zinawapatia wakulima hasara sana” Alisema Mhe. Kikwete.
Ametumia fursa hiyo kuwataka wakulima,wafugaji,wavuvi kuwatumia wataalamu wa SUA ili waweze kuwasaidia kutatua changamoto zao mbalimbali na kuwataka pia watafiti wa SUA kutoka na kuwafikia wakulima kote waliko nchini.
Akiwa katika banda hilo la SUA amevutiwa na Utafiti wa ufugaji Samaki, Aina za malisho ya mifugo, Ufugaji wa Sungura, bidhaa za wajasiliamali zinazotokana na kilimo pamoja na mfumo wa AFYADATA unavyofanya kazi.
Rais Mstaafu Dkt. Jakaya Kikwete amekuwa moja kati ya viongozi wakuu wa nchi ambao wanajishughulisha na kilimo pamoja na ufugaji na hivyo kutembelea Chuo Kikuu cha Sokoine na kwenye maonesho ya Nanenane kujifunza mbinu mbalimbali za kuboresha Kilimo na ufugaji wake.

# MHE. SIMBACHAWENE APONGEZA WATAFITI WA SUA KUTUZA VYURA WA KIHANSI

Waziri nchi Ofisi ya makamu wa Rais Muungano na MazIngira Mhe. Simbachawene amepongeza kazi kubwa inayofanywa na watafiti wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA katika kuhakikisha vyura wa Kihansi wanaendelea kuhifadhiwa pamoja na bioyoanuai zote zilizopo katika eneo hilo la Kihansi.

Pongezi hizo amezitoa wakati wa ziara yake fupi Chuoni hapo na kupata taarifa ya kazi zinazofanywa na Watafiti wa SUA kwa kushiriiana na wadau wengine katika kutunza Mazingira na viumbe katika eneo hilo la bwawa la kihansi kabla ya kutembelea kuona hali halisi katika eneo hilo.

Mhe. Simbachawene ambaye ameambatana na Mwenyekiti wa bodi ya NEMC na wataalamu wengine



kutoka Chuo kikuu cha Dar es salaam na wizara yake amesema swala kubwa linalopaswa kuzingatiwa katika kazi hiyo ni kuhakiksha zinapatikana njia endelevu za kutunza bayoanuai zote katika eneo hilo la Kihansi badala ya kufikiria kutumia fedha nyingi katika kutunza vyura peke yake.

Amewataka wataalamu hao wote kwa pamoja washiriki katika kulinda na kutunza eneo hilo kukaa pamoja na kutengeneza andiko ambalo litaonyesha faida za ujumla za utunzaji wa eneo hilo hasa nafasi ya utalii kwa watu mbalimbali wanaponda kuja kuangalia vyura hao ambao hawapatikani kokote duniani.



Katika hatua nyingine amewaagiza wataalamu wa NEMC na ofisi yake kuhakikisha wanaanza mchakato wa kupata haki miliki ya uvumbuzi na utafiti wa kahawa pori ya Kihansi ambayo imeonekana kuwa na ubora mkubwa ikilinganishwa na aina ya Arabika na Robusta ili nchi iweze kupata haki yake kabla ya watafiti wa nchi zingine kuwahi kwakuwa wanaona machapisho mbalimbali ya watafiti hao Wanayoyafanya.

Awali akiwasilisha mada fupi kuhusu kazi zinazofanywa na SUA katika utunzaji wa Vyura hao Prof. Gerald Misinzo amesema walianza kazi hiyo muda mrefu mara baada ya kugundulika kuwa idadi ya vyura hao wanatoweka na baadae serikali kuamua kwenda kuwahifadhi nje ya nchi na baada ya muda sasa vyura hao wamerudishwa nchini na kuzalishwa katika Chuo Kikuu cha Dar es salaamu na kuanza kurudishwa taratibu katika eneo hilo la Kihansi.

Dkt. Misinzo amesema kazi kubwa ya ambayo wataalamu wa SUA wamkabidhiwa ni kuhakikisha

wanaangalia magonjwa na tiba za magonjwa hayo kwa vyura ili wasiendelee kuathiriwa na kubainisha kuwa tatizo kubwa ambalo wameligundua ni magonjwa ya fangasi hivyo jitihada zinaendelea kuhakikisha wanatokomeza magonjwa hayo.

Kwa upande wake Prof. Paul Kusolwa mtaalamu wa uzalishaji wa mimea kutoka Ndaki ya Kilimo akiwasilisha furasa nyingine ambazo pia wao kama watafiti wameiona na uwepo wa aina ya kahawa pori ambayo baada ya kuifanyia utafiti kwa muda mrefu wanaona inaweza kuwa ya kipekee nay a aina yake kutokana na kuwa na sifa nzuri ikilinganishwa na hizi zilizopo kwa sasa.

Amesema tayari wameshafanya utafiti wa kina na kupata matokeo mazuri na wamewakabidhi taasisi ya utafiti wa kahawa TACRI ili waweze kuendelea zaidi hasa wakizungatia kuwa mradi huo ufadhili wake unafikia mwisho na ni lazima utafiti huo uendelee ili hatimaye tuweze kuzalisha kahawa hiyo nzuri.

Akizungumza na kumshukuru ujio wa Waziri huyo



Makamu wa Mkuu wa Chuo Prof. Raphael Chibunda amemuomba waziri Simbachawene na wataalamu wa NEMC kuona umuhimu wa kuwezesha chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA kupata maabara maalumu ambayo itakuwa na uwezo wa kufanya tafiti zote zinazohusu masuala ya mazingira nchini ikizungatiwa kuwa SUA inao wataalamu wengi wabobevu katika Nyanja hiyo.

Amesema hivi sasa wataalamu hao wanafanya tafiti zinazohusu masulaaya mazingira kwenye maabara ambazo sio maalumu kwa kazi hiyo na kujikuta wanachanganyika na watafiti wa masuala mengine mbalimbali ikiwemo kilimo hali ambayo inaweza kushusha ufanisi katika kufanya tafiti na kupata majibu ambayo yataleta tija kwa taifa.

Prof.Chibunda amemhakikishia Waziri Simbachawene kuwa Chuo kipo tayari kushirikiana na ofisi yake na ofisi zingine katika kuanzisha maabara hiyo na kufanya tafiti za kina kwa manufaa ya taifa.





# SUA YATEKELEZA AHADI YAKE KWA MHE. MAGUFULI



Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimetekeleza ahadi yake iliyoitoa kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania DKT. John Pombe Magufuli alipotembelea Chuo mwaka 2018 ya kuhakikisha inanunua babasi mawili kwa ajili ya shughuli mbalimbali za wanafunzi. Akizungumza wakati akipokea mabasi hayo leo tarehe 23 August, 2019 Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda amesema kuwa mabasi hayo mawili aina ya TATA yenye thamani ya shilingi. Mil. 406 yamenunuliwa kutokana na mapato ya ndani ya chuo. Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mabasi hayo Prof. Chibunda aliwashukuru wale wote waliohusika kufanikisha kununuliwa kwa mabasi hayo na kusema kuwa yatasaidia kutatua changamoto ya usafiri kwa wanafunzi iliyokuwa ikiwakabili kwa muda mrefu.



***"Kulikuwa kuna changamoto ya usafiri kwa wanfunzi wetu kutoka Kampasi yetu ya Mazimbu kuhudhuria masomo hapa Kampasi kuu pamoja na wale wanaoenda kwenye Mafunzo kwa vitendo, hivyo naamini magari haya yatapunguza kama sio kutaua changamoto hiyo"*** alisema Prof. Chibunda.

Aidha, Prof. Chibunda alitoa wito kwa madereva, mafundi, wanafunzi pamoja na wafanyakazi kuyatunza mabasi hayo na kuhakikisha yanatumika kuleta maendeleo na wepesi wa utendaji kazi kwa vitendo kwa wanafunzi na chuo kwa ujumla. Akiongelea juu ya ujio wa mabasi hayo, Naibu Makamu wa Mkuu wa Chuo (Utawala na Fedha), Prof. Fedrick Kahimba amesema kuwa mabasi hayo yatapunguza gharama ambayo iliyokuwa inatumika hapo awali kutokana na maboresho ya mabasi ambayo yaliyokuwepo kabla, hivyo ameagiza madereva na wanafunzi kuhakikisha kuwa watatumia vizuri na kwa kuyatunza ili kuleta tija husika ndani ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, SUA. Akihitimisha kwa kutoa shukrani kwa Uongozi wa Chuo kwa kupokea na kuzindua mabasi hayo, Naibu Makamu wa Mkuu wa Chuo (Utawala), Prof. Peter Gillah amesema kwamba mabasi hayo yatatatua changamoto ambayo ilikuwa ikiwapata wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, SUA hasa wale ambao wanatakiwa kusoma na kufanya mazoezi ya vitendo kutoka Kampasi ya Solomon Mhalangu hadi Kampasi Kuu ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA.

# UONGOZI WA KIWANDA CHA SUKARI CHA MTIBWA WAPONGEZA WAHITIMU WA SUA WANAOWAAJIRI

Mkurugenzi Mkuu wa Kiwanda cha Sukari Mtibwa bwana Stan Rau amepongeza Chuo kikuu cha Sokoine cha kilimo SUA kwa elimu bora wanayoitoa kwa wanafunzi wake na hivyo kufanya vizuri kwenye maeneo mbalimbali ambayo wameajiriwa.



Mkurugenzi huyo ametoa pongezi hizo wakati akizungumza na Uongozi wa Chuo kikuu cha SUA alipofanya ziara ya siku moja katika chuo hicho akiambatana na timu ya wataalamu wake kwa lengo la kujifunza na kuona huduma mbalimbali ambazo zinatolewa na Chuo. Bwana Rau amesema asilimia kubwa ya wataalamu wake wa kilimo ni wanafunzi wa SUA na wamekuwa na mchango mkubwa katika kusaidia kiwanda kuzalisha miwa yenye ubora na kutoa huduma za ushauri kwa wakulima na wafanyakazi wengine kiwandani hapo na kuongeza tija.

Akizungumzia ugeni huo naibu makamu wa mkuu wa chuo utawala na fedha Prof. Federick Khimba amesema alisema lengo lao ni i kujifunza juu ya huduma mbalimbali ambazo zinapatikana chuoni ikiwemo maabara za chakula na udongo ambazo zitaweza kuwapunguzia gharama za kupeleka sampuli za bidhaa zao kwenye nchi za kigeni kwa ajili ya vipimo mbali mbali. Prof. Kahimba amesema ujuio huo ni fursa nzuri ya kuanzisha ushirkiano wa karibu kati ya Kiwanda na Chuo na hivyo kuwezesha wanafunzi na watafiti wa SUA kutumia kiwanda hicho katika kufanya mazoezi na tafiti mbalimbali ambazo zitasaida kuongeza tija katika uzalishaji wa sukari nchini. Amesema kupitia ushirkiano huo utasaidia wanafunzi wa SUA kupata ajira kwenye Kiwanda cha Mtibwa na Kagera chini ya kampuni ya Super Doll lakini pia kuwapa fursa waajiriwa wapya kufanya mafunzo kwenye viwanda hivyo ili wanaporudi kuanza kufundisha waweze kufundisha vitu ambavyo kweli wanavijua vizuri.





## SUA YANG'ARA MAONYESHO YA WAKULIMA NANENANE 2019

**C**huo kikuu cha sokoine cha kilimo SUA kimepata cheti na Vikombe kwenye maonesho ya wakulima nanenane kwa mwaka 2019 Kitaifa Mkoani Simiyu na Kikanda Mkoani Morogoro. Kwa mujibu wa Waandaji wa maonesho hayo SUA imeibuka mshindi wa pili kwa upande wa taasisi za elimu ya juu na mafunzo ya ufundi kitaifa Mkoani Simiyu na Mshindi wa Pili pia kwenye maone-



sho ya kanda ya Mashariki Mkoani Morogoro yaliyoanza tarehe 1 – 8 mwezi wa nane mwaka 2019. Chuo kikuu cha Sokoine kilionesha teknolojia na mbinu mbalimbali za kuvutia za kilimo na ufugaji zikiwemo kwenye Usindikaji wa mazao ya kilimo, bidhaa za ngozi,Panya wanaotambua mabomu na TB,Vifaa vya kupima udongo vinavyohamishika,Uzalishaji wa mimea,Mbegu za miti na mbao, Ufugaji kuku wa Kienyeji, Teknolojia ya AFYADATA nyingine nyingi ambazo zinafanywa na watafiti wa Chuo kikuu cha Sokoine.

